



Australian Government

COVID-19 VACCINATION

Hatua 6 za kuidhinisha chanjo



Nchini Australia, **Utawala wa Bidhaa za Matibabu (TGA)** unaidhinisha chanjo zote kabla kuweza kutumiwa.



TGA ni sehemu ya Idara ya Afya ya Serikali ya Australia.



TGA inahakikisha dawa tunazotumia nchini Australia:

- ni salama
- inafanya kazi vizuri.



TGA wakati wote inafuata hatua 6 zile zile ili kuidhinisha chanjo nchini Australia.

Hatua ya 1 – Kabla ya kufanya maombi ili chanjo kuidhinishwa



Kuna kampuni nyingi kote ulimwenguni zinazotengeneza chanjo.

Kampuni zinapaswa kuomba kutoka TGA ili chanjo yao kuidhinishwa.



Kabla kampuni kuweza kupeleka maombi kwa TGA, kampuni lazima iambie TGA:

- kuhusu chanjo inayotaka kuidhinishwa



- sababu watu wanahitaji chanjo
- majaribio ya kliniki ambayo imeendesha.



Jaribio la kliniki ni utafiti ili kuchunguza kama chanjo:

- ni salama
- inafanya kazi vizuri vizuri.



Kampuni lazima pia iambie TGA jinsi itahakikisha mbeleni chanjo yake:

- ni salama
- inafanya kazi vizuri.

Ikiwa TGA inamua kampuni imetengeneza chanjo kwa njia sahihi, itaiambia kuweka maombi.

Hatua ya 2 – Maombi ya kuidhinishwa chanjo



Kampuni lazima ipeleke maombi kwenda TGA ili chanjo yake iweze kuidhinishwa.



Wakati inapoomba, kumpani inapaswa kuiambie TGA:

- jinsi majaribio ya kliniki yanaonyesha chanjo ni salama na inafanya kazi vizuri
- jinsi viungo katika chanjo ni salama



Kampuni lazima pia iambie TGA:

- jinsi itakavyotengeneza chanjo
- ikiwa kuna hatari zozote kwa watu wanopata chanjo.

Hatua ya 3 – Kuangalia maombi



TGA itaangalia kwa uangalifu:

- chanjo ili kuhakikisha ni salama
- maelezo yanayotolewa na kampuni.



TGA:

- itafanya kazi na wataalam wengine kuhakikisha kuwa chanjo ni salama



- itaangalia kila kiungo ndani ya chanjo ili kuhakikisha kuwa ni salama.



TGA pia:

- itaangalia majaribio ya kliniki kuhakikisha kuwa chanjo ni salama kwa kila mtu nchini Australia.



- itahakikisha kuwa chanjo inakidhi viwango vya Australia.



- itaangalia ni jinsi gani nchi nyingine kote ulimwenguni zimetumia chanjo.



TGA inaweza pia kuuliza kampuni maswali yoyote zaidi ikihitajika.

Hatua ya 4 – Kuamua uamuzi



TGA inaamua kama itaidhinisha chanjo.



Ikiwa TGA inaidhinisha chanjo, basi itaidhinisha kwa muda wa miaka 2.

Baada ya miaka 2, kampuni inaweza kuomba TGA kuidhinisha chanjo hadi ya miaka 6 zaidi.

Hatua ya 5 – Kuandikisha chanjo



Baada ya TGA kuidhinisha chanjo, itaiongeza katika Rejesta ya Bidhaa ya Matibabu ya Australia (yani Rejesta).



Rejesta ni kumbukumbu ya chanjo zote ambazo TGA imeziidhinisha nchini Australia.

Rekodi inajumuisha:

- jina la kampuni
- jina la chanjo
- viungo ambavyo vimo katika chanjo
- maelezo kwa watu wanaopata chanjo.



Baada ya chanjo kuongezwa katika Rejesta, kampuni inaweza kuanza kusambaza chanjo.

Hatua ya 6 – Kufuatilia chanjo



TGA itaendelea kuangalia chanjo wakati watu zaidi wanazidi kuipata.



Hii inatokea ili kuhakikisha:

- bado ni salama
- bado inafanya kazi vizuri.



Ikiwa kuna matatizo yoyote, TGA inaweza:

- kuchunguza tatizo na chanjo yenyewe
- kuwapa watu habari mpya kuhusu jinsi chanjo ilivyo salama
- kuondoa idhini, ikiwa inahitajika.

Habari zaidi



Unaweza kutembelea tovuti ya Idara ya Afya kwa www.health.gov.au/covid19-vaccines-languages kupata habari zaidi juu ya chanjo katika lugha yako.



Unaweza kupiga simu kwa Simu ya Msaada wa Coronavirus ya Kitaifa kwa **1800 020 080**.

Ikiwa unahitaji habari katika lugha mbali na Kiingereza, pigia simu kwa Huduma ya Utafsiri na Ukalimani kwenye **131 450**.